



# USAID

KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



UN Women Tanzania  
Maoni yangu ni muhimu

## TANZANIA WANAWAKE WANAWEZA

USAID inatoa msaada kwa Mradi wa UN Women wa Uongozi na Ushiriki wa Wanawake katika Siasa wa Awamu ya Pili unaojulikana kama Wanawake Wanaweza. Mradi huu unakuza usawa wa kijinsia, ushiriki wa kisiasa, na uwezeshaji wa wanawake kuweza kupata nafasi muhimu za uongozi. USAID inakusudia kuhakikisha kuwa wanawake wanaongoza na kushiriki katika michakato ya kisiasa na uchaguzi-kama wapiga kura, wagombea, na wawakilishi waliochaguliwa. Mradi utaimarisha uwezo wa wanawake kama viongozi, haki zao chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kanuni za kimataifa za haki za binadamu na wanawake zinazosilitiza kuhusu wanawake kushiriki kwa usawa katika utawala wa demokrasia, kama viongozi na chachu ya mabadiliko.

Mchango wa USAID kwa UN Women unazingatia:

1. Kuunda na kujenga uwezo wa kada la wanawake wenye nia, uwezo na sifa za uongozi.
2. Kuongeza uwezo wa kitaalam wa wanawake ili wajihusishe na michakato ya kisiasa na uongozi

Mchango wa USAID katika Mradi wa Wanawake Wanaweza utawezesha na kuendeleza ushiriki wa wanawake katika uongozi, na siasa kwa kutambua na kuimarishe uwezo wa wanawake watia nia.

## **MRADI UTALENGA:**

- Kuimarisha uwezo wa viongozi wanawake katika uongozi wa mabadiliko, ustadi wa mawasiliano, kuandaa kampeni, uandaaji wa bajeti na jinsi ya kupata wafadhili, na utatuzi wa migogoro ili kuongeza nafasi zao za kuteuliwa kama wagombea na kuchaguliwa.
- Kuainisha vizuizi ambavyo vinazuia uteuzi wa wanawake katika vyama vyaa siasa na kufaulu kwenye kampeni.
- Kuendeleza na kupanua mitandao ya kitaaluma, asasi za kiraia, na mitandao ya kijamii ili kukuza na kudumisha uchaguzi wa wanawake pamoja na kubaini viongozi wanaouna mkono juhud hizi ndani ya vyama vyaa siasa, jamii na vikundi vyaa vijana.
- Kufanya kazi na viongozi wanawake waliopo kama washauri na vielelezo vyaa kuwatia moyo na kuwasaidia wanawake, pamoja na wanawake vijana na wale wenye ulemavu kushindana kama wagombea wa kisiasa.

**BAJETI YA USAID** Dola za Marekani laki 5

### **MUDA**

Novemba 2018 – Disemba 2022

### **MAENEKO YA MRADI**

Nchi nzima

### **WABIA WA MRADI**

UN Women

### **WASHIRIKA MUHIMU**

Ubalozi wa Finland

Ubalozi wa Sweden

Ubalozi wa Switzerland

### **MAWASILIANO YA USAID**

Florida Henjewele

Afisa Mkataba Mwakilishi

+255 22 229 4490

[fhenjewele@usaid.gov](mailto:fhenjewele@usaid.gov)

### **MAWASILIANO YA MBIA**

Erasmina Massawe

Meneja Mradi WLPP

+255 742 486 153

### **KWA TAARIFA ZAIDI**

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)

Facebook: USAIDTanzania

Twitter: @USAIDTanzania